

**USAWIRI WA MANDHARI KATIKA RIWAYA YA  
GEREZANI  
MFANO: "HAINI" YA ADAM SHAFI**

---

**Alaa Salah Abdulwahed**

*Mhadhiri Msaidizi wa Kiswahili  
Idara ya Lugha za Kiafrika  
Kitivo cha Lugha na Ukalimani  
Chuo Kikuu cha Al-Azhar  
Misri*

Makala hii imewasilishwa kwenye  
Kongamano la Pili la Kimataifa la Kiswahili lililoandaliwa na  
Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)

Zanzibar, Tanzania  
12-13 Desemba 2018

# Usawiri wa Mandhari katika Riwaya ya Gerezani

## Mfano: "*Haini*" ya Adam Shafi

*Alaa Salah Abdulwahed\**

### *Ikisiri*

Makala hii inachambua usawiri wa mandhari; wakati na mahali katika riwaya moja ya Kiswahili ambayo kiasi kikubwa cha matukio yake yamejiri gerezani. "*Haini*" ni riwaya ya nne ya mwanariwaya mtanzania maarufu Adam Shafi, ambaye ameifanya riwaya yake hiyo kama visa vya kusimulia yaliyojiri gerezani yakiwemo mateso, maumivu na hata matamano ya kutoka nje ya mahali pa maangamizi kama hapo. Bila shaka mandhari ni mojawapo ya nguzo zinazojenga kazi yoyote ya fasihi na hasa riwaya, ambapo mwandishi hataweza kuelezea ujumbe wake pasipo na kuwa na nguzo maalumu za kujenga kazi yake. Uzoefu wa mwandishi hubainika kupitia utumiaji wake wa nguzo hizo na kuzifanya zisaidiane kwa minajili ya kufanikisha kazi yake na kuyafikisha mawazo yake kwa hadhira ya wasomaji. Riwaya ya gerezani ndio aina ya riwaya inayosimulia matukio yanayo jiri gerezani, ambapo mhusika mkuu na wahusika wengine wanateseka au wanapata adhabu ya uhalifu sawa wamefanya uhalifu huo au wameingizwa humo bila ya kufanya hatia yoyote.

---

\* Mwandalizi wa makala hii ni Mhadhiri Msaidizi wa Kiswahili, Idara ya Lugha za Kiafrika, Kitivo cha Lugha na Ukalimani, Chuo Kikuu cha Al-Azhar, Misri. Ambaye kwa sasa ni mwanafunzi wa Uzamivu unaosimamiwa kwa pamoja baina ya Chuo Kikuu cha Al-Azhar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).